Maana ya Mtu Kuanguka kutoka Juu

Lesley Nneka Arimah

Extract translated by Elias Mutani

Maana yake ni habari itakayorudiwa mfululizo masaa ishirini na nne. Ni habari ya wanasiasa wanaojaribu kutuliza hali ya mambo; au wanaharakati wanaoshinikiza maandamano. Ni habari ya mjukuu wa Francisco Furcal kuitisha kikao cha waandishi na kutetea historia na urithi ulioachwa na ukoo wake.

"Kanuni aliyotunga babu yangu bado inafanya kazi. Hisabati imekamilika na haibadiliki. Hitilafu zinazoibuka ni matokeo ya kasoro zinazosababishwa na watu wanaofanya makosa katika kukokotoa."

Kosa kubwa. Na lingepelekea watu kujihami, kujiweka mbali na vyeti vyao, mbali na matokeo yao ya mitihani, na kila kitu kilichoonesha walikuwa watu wenye akili sana. Nneoma alijaribu kukumbuka ni wapi alipoacha vyeti vyake baada ya kosa kutokea, lakini lilimsaidia kutafakari ni wapi anatoka, na kumfanya awakumbuke wale aliowaacha nyuma yake.

Hakutaka kubahatisha. Alituliza akili yote kwenye picha isiyoonekana vema, iliyorekodiwa kwa kamera ya ulinzi. Kifaa-mwendo kilikuwa kimenasa futi hamsini za mwisho alizomalizia mtu mmoja kuanguka, mikono iliyorushwa kwa tahamaki kama pangaboi, na mwili uliotanda chini ukiwa umechanua mikono na miguu yake. Wanahabari wakawageukia Wanahisabati waliovumbua kanuni ya kupaa. Waliwavizia katika sherehe, walipokwenda kuwachukua watoto wao kwenye magari yao meusi yenye kung'ara, kwenye mapumziko yao, walipokuwa wakipata starehe zilizokuwa adimu machoni mwa wengi waliokuwa wakiwatazama, ambao wangefurahi kuona nyuso zile zikiingia aibu na vinywa vile visivyojua njaa vikitoa maneno ya kujitetea.

Kwa kitendo cha kuwalaumu Wanahisabati badala ya kanuni, Martina Furcal na Kituo chake walizusha mvurugano miongoni mwa wanasayansi hawa waliodhaniwa hawawezi kukosea ili kulinda historia ya jina la ukoo wake. Na mali alizorithi. Pengine halikuwa kosa baya sana.

Nneoma aliendelea kuangalia vituo mbalimbali vya runinga na kusikiliza kwa makini. Endapo uvumi kuwa kanuni ya Furcal imeanza kujulikana kila kona na kupata mwitikio, hatimaye itasambaa na kuwafikia Wanahisabati 2,400 kama yeye wanaozunguka dunia na kuendesha maisha yao kwa kukokotoa na kuondoa mihemko, wakiichota kutoka kwenye miili ya watu walio hai, mithili ya kuondoa sumu toka kwenye kidonda.

Mwanamke huyu alikuwa miongoni mwa Wanahisabati 57 waliosajiliwa na kubobea katika ukokotozi wa simanzi kubwa, idadi iliyopungua toka 59 waliosajiliwa mwaka uliotangulia. Alvin Claspell, kutoka Australia, alijiua kwa kuwa, kama simulizi zinaweza kuaminika, alipata kichaa na kutaka kula mwili wake. Kumbe hii haikuwa kazi ambayo mtu yeyote angeweza kuifanya. Na Kioni Mutahi naye pia alitoweka, na kuiacha New Kenya kubaki na mtaalamu mmoja tu wa masuala ya simanzi.

Walikuwepo wafanyakazi sita wa masuala ya simanzi katika Muungano wa Biafra na Britannia ambako ndipo Nneoma anaishi kwa sasa, ukiwa ni uwiano mkubwa kuliko yote wa wafanyakazi wa simanzi katika eneo lenye uwiano mkubwa wa wagonjwa wa simanzi kupita maeneo yote. Tena uwiano mkubwa unaolipa.

Habari ile ilitangazwa tena na tena. Nneoma alizima runinga. Kelele zote zingekwisha endapo tu wataalamu wa kuruka wangetumia akili na kumtupia lawama yule bwana aliyedondoka kuwa alifanya makosa katika kukokotoa. “Ficha aibu yako,” ndivyo usemi mmoja wa Kimarekani usemavyo, ingawa ni wachache tu wenye kuutumia tena katika bara hilo.

Kioo cha simu kilitoa ishara ya kupokea ujumbe. Nneoma alifanya haraka kubonyeza kitufe cha kupokelea, akiwa amejaa shauku, iliyomfanya kuona aibu, na aliona aibu zaidi alipogundua kuwa hakuwa Kioni aliyetuma ujumbe ule bali ni msaidizi wake aliyemkumbusha kuwa ana kipindi cha kufundisha shuleni. Aliufuta ujumbe ule – alikuwa anakumbuka – na aliudhika. Kwa mara nyingine tena aliwaza kumfuta kazi yule msichana. Lakini kuna nyakati unahitaji mtu wa kukusaidia, mfano pale rafiki yako wa kike anapovunja uhusiano kwa sauti ile ile ya upole na ukarimu aliyoitumia kuanzisha uhusiano huo, na kukuacha ukifungasha virago na kuhamisha takataka ulizokusanya kwa miaka mitatu ndani ya juma moja. Wasaidizi hufanya maisha kuwa mepesi. Lakini yalikuwa ni majuma nane tu yamepita na Nneoma alikwisha sahau. Kabisa.

Alikusanya makabrasha yake na kumpigia simu dereva. Kufumba na kufumbua gari lilifika na kuegeshwa mbele ya mlango wa kioo. Amadi alizoea kufanya haraka namna ile, na ndivyo ilivyokuwa, tangu Nneoma alipokuwa mtoto. Mama yake alizoea kusema kuwa aliweza kupiga simu alipokuwa akiteremka ngazi na alipofungua mlango alimkuta Amadi akiwa tayari, anamsubiri. Mama alikwisha tangulia na baba yake aliyekuwa hajiwezi alikuwa hatoki tena nyumbani. Amadi alimhudumia baba yake hadi pale Nneoma aliporejea kutoka New Kenya. Ndipo baba yake alipomtoa Amadi kama zawadi kwake, kama vile atoaye kapu la jibini. Nneoma alimtwaa dereva yule, akijua ilikuwa ni sadaka ya amani. Na ingawa maisha hayakuwa tena kama zamani, alimtembelea baba yake kila Jumapili aliyofuatia.

Nneoma alimwelekeza Amadi ampeleke madukani. Walikatiza mitaa mipana ya Enugu na kupita uwanja wa michezo uliofurika watoto wa kizungu waliotiririka jasho. Si kwamba alikuwa amejenga kisirani kwa Waingereza bali aliambukizwa kidogo tu na baba yake, aliyekuwa mkali. Baba yake aliwachukulia zaidi kama wakimbizi kuliko washirika na kwa muda mrefu hakuchangamana pamoja nao.

"Hawakuwa na nchi yao walipokuja hapa na wamejaribu kupora kila kitu, tena hawachangii chochote." Ndivyo alivyozoea kusema.

Hii haikuwa kweli kabisa.